
EE BWANA UNIPOKEE

BEN BOSCO
St.Joseph Choir
University of Dodoma
13 october 2024
Mobile:+255755630683



2.Najongea karamuni,unipe yako mapendo(ee Bwana),naja upesi nipokee/
Kwako ninakimbilia,salama ya moyo wangu(ee Bwana),ndiwe sitara yangu Bwana.

3.Uniponye majeraha,tabibu wangu wa kweli(ee Bwana),wewe ni tumaini langu/
Unioshe dhambi zangu,nitakate niwe safi(ee Bwana),niwe mpya kama theluji.

4.Yesu yupo hadanganyi,yupo hapa kwa mafumbo(mafumbo),ya mkate na ya divai/
Nami nasadiki kweli,bila hofu namwabudu(ni Bwana),nampa mapendo ya kweli.

5.Alikufa msalabani,ili tupate wokovu(wokovu),kwa kuficha umungu wake/
Na ubinadamu wake,ameficha altareni(ni Bwana),nami nasadiki ya kweli.

6.Yesu wangu nakuita,uje kwangu mwamba wangu(ee Bwana),mimi niwe wako daima/
Ukae nami milele,siku zote za maisha(ee Bwana),ndiwe furaha yangu kweli.

7.Wewe ni faraja yangu,katika mahangaiko(ee Bwana),kwangu ni tulizo la moyo/
Hata niwapo shidani,wanipa mkono wako(ee Bwana),wewe ni rafiki wa kweli.

8.Pendo lako lanukia,kwa harufu nzuri nzuri(ee Bwana),mithili ya ua la konde/
Lachanua linang'ara,latiririsha baraka(baraka),nalo ni pendo la ajabu.

9.Mariamu we bikira,nipeleke kwa mwanao(mwanao),niishi nayeye milele/
Maria uniombee,nipate zake baraka(baraka),na neema neema zake.

benedictobosco675@gmail.com